JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

SHULE YA SEKONDARI KIBAKWE
S.L.P 243
MPWAPWA
29/03/2022

Simu ya Mkononi:
Mkuu wa shule 0784-221038
Makamu wa mkuu wa Shule 0684-131877

KUMB.NA:/ED/KSS/JI/03/2022

Kwa Mzazi wa:……..
……
……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022 SHULE YA SEKONDARI KIBAKWE.

Napenda kukuarifu kuwa kijana wako amechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Kibakwe Kidato cha Tano mchepuo wa ……mwaka 2022. Nakupongeza sana kwa kijana wako kufaulu na hatimaye kujiunga na shule hii.

Shule itafunguliwa tarehe **05 Septemba 2022** na ndiyo siku ambayo kijana wako anatakiwa awe ameshafika shuleni Endapo mwanafunzi atachelewa kuripoti kwa zaidi ya **siku 7 kuanzia tarehe ya kufungua Shule** nafasi yake itachukuliwa na wanafunzi wengine.

A.MAHALI SHULE ILIPO:

Shule yetu ipo Mkoa wa Dodoma, Wilaya ya Mpwapwa, jimbo la Kibakwe. Mji wa Mpwapwa unafikika kwa mabasi ya moja kwa moja kutoka Dodoma. Upo usafiri wa kila siku kutoka Dodoma ambao hufanya safari zake kuanzia saa 03:00 asubuhi na saa 09:00alasiri. Usipopata usafiri wa aina hii, unaweza kupanda mabasi yanayoelekea Gairo, Morogoro au Dar Es Salaam na kushuka kituo cha ***Mbande***, mahali ambapo ni njia panda ya kuelekea Mpwapwa na Kongwa. **Tafadhali sana usipande gari au basi linaloekea Kongwa, subiri linaloelekea Mpwapwa.**

Endapo unatokea Dar Es Salaam au Morogoro unashauriwa kutumia basi lolote kati ya mabasi yanayofanya safari zake kuja Mpwapwa moja kwa moja; usafiri huu upo kila siku,ukikosa basi la moja kwa moja tumia basi lolote linaloelekea Dodoma na uteremkie Mbande na kupata usafiri wowote unaolekea Mpwapwa. **Unatahadharishwa tena kutotumia magari yanayoishia Kongwa.**

Kwa wale watakaotumia usafiri wa treni, tunashauri kuteremkia Dodoma mjini ambapo ni rahisi kupata usafiri wa kuelekea Mpwapwa mjini moja kwa moja. Mabasi yanayokuja Mpwapwa huanzia safari zake Dodoma Mjini kwenye kituo kiitwacho ***SOKO LA NDUGAI.***

Mara ufikapo kituo cha mabasi Mpwapwa utapanda magari yanayokwenda Kibakwe ni kilomita 50 kutoka Mpwapwa mjini. Mabasi ya kwenda Kibakwe yapo hadi saa kumi jioni, hivyo unashauriwa kuanza safari mapema ili kufika mapema Kibakwe. Ukifika kituo cha mabasi Kibakwe ulizia shule ilipo ni mwendo wa dakika 10 kutembea kwa miguu.

N.B. ***KUNA BASI LA ALYSAID,NYEMBELA NA NGASERE KUTOKA DSM HADI KIBAKWE MOJA KWA MOJA.NA BASI LA ARUSHA EXPRESS KUTOKA ARUSHA HADI MPWAPWA***

Tafadhali sana katika kumleta au kumsafirisha kijana wako zingatia sana siku na muda wa kazi.(Siku za Jumamosi, Jumapili na Sikukuu za Kitaifa siyo siku za kazi)

Ukiwa umetimiza maagizo yaliyoko kwenye barua hii mtoto wako atapokelewa kwa Mkuu wa shule ambaye atamsajili hatimaye kuanza masomo.

B.MICHANGO MBALIMBALI

01. Ada ya shule kwa mwaka (Tshs 35,000/= kwa muhula)…….……Tshs 70,000/=
02.Fedha ya tahadhari (hairudishwi)…….…...……...Tshs 5,000/=
04. Mchango wa Taaluma…….. Tshs 20,000/=
05. Mchango kwa ajili ya ulinzi na wapishi na vibarua wengine ……Tshs 30,000/=
06. Kitambulisho…… Tshs 6,000/=
07. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza (Tsh 5,000/ kwa ajili ya kujiunga na mfuko wa bima ya afya CHF.
08.Ukarabati wa samani……Tshs 15,000/=
09. Mtihani wa kujipima 25,000/=

JUMLA YA GHARAMA NI 181,000/=

Fedha zote ziwekwe kwenye akaunti ya shule **NMB** namba **50401100039 (KIBAKWE SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTION).**

Akaunti hiyo ni ya NMB. Andika jina la mwanafunzi kwenye bank-pay-inslip na kuja nayo shuleni(bank-pay-inslip original tu ndiyo itapokelewa shuleni na siyo photocopy) "**HATUPOKEI FEDHA TASLIMU"**

C.TAALUMA:

Katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaendeleza ufaulu waliokuja nao hapa shuleni kila mwanafunzi anatakiwa kufaulu vizuri kila somo kwa kiwango ***kisichopungua alama 55***. Endapo atashindwa kufikia alama hizo katika mitihani au majaribio mawili mfululizo itabidi mzazi au mlezi uliyeandikishwa uje shuleni kushauriana na uongozi wa shule njia sahihi ya kumsaidia kijana wako. "**Shule ya sekondari Kibakwe bila daraja la tatu, nne na sifuri inawezekana timiza wajibu wako"**

D. VIFAA VYA KUJA NAVYO:

01. Bunda moja la karatasi ya photocopy (A4) kwa matumizi ya mazoezi na mitihani ambayo itatolewa kila muhula wa masomo.
02. Picha 04 (nne) za "*Passport size "*kwa matumizi ya ofisi.
03. Raba, T-Shirt 2 za rangi nyekundu mpya kwa ajili ya michezo na muda usiyo wa darasani.
04. Kalamu na Daftari **(counter books)** za kutosha kulingana na masomo yaliyo kwenye mchepuo
05. Jembe jipya lenye mpini, mfagio wa ndani na nje,kwanja na brashi kwa ajili ya usafi wa vyooni 1.
06. Godoro lenye ukubwa wa futi mbili upana na urefu futi sita.
10. Orodha ya vitabu ambavyo anatakiwa kuwa navyo imeambatanishwa.
11. Dissecting kit kwa wanafunzi wa **CBG**
12. Scientific calculator kwa wanafunzi wa **CBG na HGK**

NB:Ili kuwa na sare moja inayofanana kwa wanafunzi wote na sisi walezi kuweza kurahisisha suala letu la malezi T shirts zinapatikana Mpwapwa Mjini kwa ndugu Sisty Karia wa namba 0784 427 439.

E.SARE YA SHULE:

1.WASICHANA;

Shati/blauzi nyeupe mbili za tetroni ya mikono mifupi, sketi mbili za heshima za rangi ya dark blue zenye malinda **14 hadi 16** na urefu hadi kwenye kisigiono **na siyo kushona V box** ,viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba (vya kupigwa na rangi) na sweta la rangi ya dark blue na soksi nyeupe***.Muislamu akiona inafaaa " hijab'' inaruhusiwa ambayo atavalia na sketi ndefu inayofika kwenye kisigino yenye marinda 14-16 . Jacket haliruhusiwi kabisa.***

N.B Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare hii atakapoanza safari yake ya kuja shule ya sekondari Kibakwe

3. SARE BAADA YA MASOMO:

Baada ya masomo utavaa sketi ya **KIJANI RANGI YA JANI LA MGOMBA YENYE MARINDA 14-16 NA UREFU HADI KWENYE KISIGIONO**. Tracksuit ya rangi ya blue wakati wa michezo na usiku wakati wa Maandalizi ya jioni.

N.B: tracksuit ni lazima kuja nayo.

Nguo nyingine ambazo siyo sare za shule haziruhusiwi kabisa zingatia hili

4. VIFAA VINGINE: Vifaa vingine ni kama ifuatavyo:

i. Shuka mbili rangi ya bluu na rangi ya pink (lazima) yatatandikwa kwa utaratibu ambao utaukuta
ii.Mto kwa ajili ya kulalia.
iii.Sanduku (trunk) imara la kuhifadhia mali yake kwa usalama bwenini.
iv. Vyombo safi vya chakula ,sahani, bakuli, kikombe na kijiko.
v. Ndoo mpya ya plastiki ya lita 10 yenye mfuniko kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kuoga, kufulia na matumizi mengine binafsi.
vi. Galoni au chombo kidogo cha kuhifadhia maji ya kunywa.
v. Blanketi **(huwa kuna baridi wakati wa usiku kwa baadhi ya miezi)**

*Mwanafunzi **HARUHUSIWI KUMILIKI SIMU YA MKONONI** hapa shuleni.Tafadhali sana tenasana na kwa heshima kubwa mzazi/mlezi mwenzetu usimruhusu kijana wako kuja nayo simu ya mkononi kwa namna yeyote ile. Kumruhusu kuja nayo ni kumtafutia matatizo kama inavyojieleza katika sheria za shule ambazo nimekuletea mzazi ili uzisome na kuzijadili na kijana wako.*

MZAZI UNATAKIWA KUMFUNGULIA MTOTO WAKO AKAUNT ILI IWE RAHISI KUMTUMIA FEDHA ZA MATUMIZI HATUPOKEI FEDHA KWA NJIA YA SIMU BANK ZILIZOPO HUKU NI NMB PAMOJA NA CRDB.

Mwanafunzi afike na barua hii pamoja na fomu ya kukubali kujiunga na Shule ya Sekondari Kibakwe na cheti cha Daktari wa hospitali ya Serikali kuthibitisha afya yake (**tafadhali usifiche kama mwanao ana tatizo la kiafya)** na Results slip ya Kidato cha Nne.Vitu hivi pamoja na vingine alivyoagizwa atavionesha au kuvikabidhi wakati wa kuripoti Shuleni.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KIBAKWE

Motto wa shule ni "ELIMU NA KAZI"

…..……..

SAJIGWA G.N

MKUU WA SHULE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE YA SEKONDARI KIBAKWE

Shule ya Sekondari Kibakwe inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 pamoja na marekebisho yake. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Kijana anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na kupewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi/walezi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa jumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu na lazima.
c. Kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni(Night Preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili pamoja na mazingira ya shule kwa jumla.
g. Kuvaa vizuri huku ukiwa umechomekea sare ya shule wakati wote.
h. Kuzingatia ratiba yote ya shule wakati wote kuanzia asubuhi wakati wa kuamka hadi usiku wakati wa kwenda kulala.
i. Mwanafunzi haruhusiwi kuvuta sigara, kufuga kucha na nywele ndefu wala kusuka.
j. Ni lazima mwanafunzi aheshimu na kukubali tofauti za ki dini, ki utamaduni na siasa zilizomo katika jumuiya yetu.

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kijana kufukuzwa shule:

01. Wizi
02. Uasherati na ushoga
03. Ubakaji
04. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocane, mirungi, kubeli nk
05. Kupigana au kupiga, kutukana au kutukanana na mtu/mwanafunzi yeyote yule
06. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
07. Kudharau Bendera ya Taifa au/na Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Shule.
08. Kuoa au kuolewa au kuwekwa kimada
09. Kumpa mimba msichana,kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
10. Kutoa mimba
11. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au/na watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi
14. Kuwepo nje ya shule muda wowote ule wa shule bila kibali cha kumruhusu kutoka nje (kutoroka)

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIBAKWE

A. Mimi mwanafunzi……...(majina matatu) wa SLP;…….nimesoma maagizo ya kujiunga na Shule ya Sekondari Kibakwe pamoja na Sheria na Kanuni zake. Nimeelewa vema nami naahidi kuwa mtiifu na mwaminifu wakati wote nitakapokuwa shuleni na mahali pengine popote. Nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu wote na nisome kwa bidii ili nipate elimu bora. Nitakuwa mfano mzuri wa kuigwa kwa ajili ya maendeleo yangu,ya shule na Taifa zima kwa jumla.

Sahihi …… Tarehe:……/……/ 20….

B. Mimi…….……....Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi: …….nimesoma maagizo ya kujiunga na Shule ya Sekondari Kibakwe pamoja na sheria na kanuni za shule. Naahidi nitamsaidia \ mwanafunzi huyu kwa hali na mali ili aweze kukamilisha masomo yake ya sekondari bila kipingamizi chochote.

Na nipo tayari kufikishwa kwenye vyombo vya dola endapo nitashindwa kumtimizia kijana wangu mahitaji yake ya msingi yaliyoorodheshwa kwenye barua ya kujiunga na Kidato cha Tano. Na maandishi haya yatumikekama ushahidi dhidi yangu.Nitashirikiana na Uongozi wa Shule ili kutimiza azma hii. Kama sitapatikana tafadhali wafuatao (ndugu watatu) waitwe shuleni pakitokea tatizo au kitu kingine chochote kitakachohitaji uwepo wangu.

Ndugu wa kwanza ……. picha

Namba ya simu ……

Uhusiano wake na mwanafunzi(kaka,dada,shangazi,mjomba,shemeji…)
…..……

Ndugu wa pili…….

Namaba ya Simu ……

Uhusiano wake na mwanafunzi……

Ndugu wa tatu …….

Namba ya Simu……
Uhusiano wake na mwanafunzi……

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MPWAPWA DISTRICT COUNCIL

MEDICAL EXAMINATION FORM
FROM HEADMASTER KIBAKWE SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 243, MPWAPWA

TO THE MEDICAL OFFICER

NAME OF STUDENT:……..……..AGE…….

MEDICAL HISTORY

	YES	**NO**
Tuberculosis		
Asthma		
Heart disease		
Jaundice		
Peptic ulcers		
Epilepsy		
Diabetes mellitus		
Kidney problem		
Anaemia		
Neurosis		

PHYSICAL EXAMINATION:
Respiratory system -
Cardiovascular system -
Gastrointestinal system -
Urinary system -
Reproductive system -
Eye: R:-
L:-
E.N.T-

INVESTIGATION
1. Blood -HB……
-WBC…….
-ESR……
-VDRL Test……
2. Urine – Pregnancy……..
-Sed……
-Stool…….

I have examined the above student and considered that he/she is physically and mentally fit/ not physically and mentally fit for further studies.

Signature…….. Designation;…….

Station;…… Date;……

ORODHA YA VITABU WANAVYOTAKIWA KUNUNUA WAZAZI.

IDARA YA KISWAHILI

1. VITABU VYA UCHAMBUZI USHAIRI

JINA LA KITABU

Kimbunga - H. Goro
Fungate ya uhuru - M.S. Khatibu
Chungu tamu - T.A. Mvungi

RIWAYA

- **Vuta nkuvute** - S.A. shafi
- **Usiku utakapokwisha** - M. Msokile
- Mfadhili - H. Tuwa

TAMTHILIYA

- **Morani** - E. Mbogo
- **Nguzo mama** - P. Muhando
- **Kivuli kinaishi** - S. Mohamedi

2. **Kiswahili Sekondari** - kidato cha V & VI - Oxford.

3. **Kiswahili Sekondari — Kidato cha Tano (TIE)**

4. Kiswahili Sekondari — Kidato cha Sita (TIE)

ENGLISH DEPARTMENT

LANGUAGE — I -

1. Ashel, N. (2009) **Advanced Level English A practical Approach**. DSM.

2. Kadeghe, Michael (2011) **The real English Textbook for Advanced Level** (form Six) - DSM

3. Kadeghe, Michael (2011) **The real English Textbook for Advanced Level** (form five) — DSM.

4. English Language for Secondary Schools, Language & Usage — Form Five & /six (TIE) papers.

5. Advanced English Language: Form Five & Six by Oxford.

LANGUAGE —II-

1. Ashel, N.(2011), **Advanced Level Literature**. The Essential Guide; Good Book Publishers, DSM.

2. **Advanced Level Literature**, (2008), Nyambui Nyangwine Publishers, DSM.

3. Achebe, A.(1966) **A man of the People**.

4. Ayi Kwei Armah (1968), **The Beautyful Ones Are Not Yet Born.**

5. Ibsen, H. (1882), **An Enemy of the People,** EA-DSM

6. Imbuga, FC(1976) **Betrayal in the City.**

7. Mirii Ngugi & Thingol (1982), **I Will Marry When I Want**, EAEP, DSM.

8. Institute of Education, **Selected Poems**.

9. Mloka, C. (2007) **The Wonderful Surgeon.**

10. English Language for Secondary Schools, Literature & Stylistics — Form Five & Six (TIE). Paper 2.

READING LIST FOR HISTORY ONE.

1. Hallert, R.(1983). **Africa Since 1875 Vol.3. East African Educational Publishers**. Nairobi, Kenya.
2. July, R.W. (1992). **A History of the African People**, East African Educational Publishers, Nairobi, Kenya.
3. Illife, J. (1995). **Africans, the History of the Continent** . Edinburg, Cambridge; University Press, London UK.
4. Manning, P. (1990). **Slavery and African Life; Occidental Oriental and African Slave trade**, Cambridge University Press.
5. Njiro, E. (1989). **A History of Africa in the 19th century**. Literature Bureau Nairobi, Kenya.
6. Rodney, W. (1976). **How Europe underdeveloped Africa**, Publishing House, Dar es salaam, Tanzania.
7. Shillington, K. (2004). **History of Africa**. MacMillan Publishers. Hong Kong, Japan.
8. Davidson, E. ef al (1997); **The growth of the African civilization East and Central Africa to the late 19th century**, Longman Group Limited, Singapore.
9. Freud, B. (1998): **The making of contemporary Africa; The Development of African societies since 1800**, Colorado, Lynne Rienner Publishers.
10. Kimambo, I and Temu, A (1969); **A History of Tanzania**, East Africa Publishing House Nairobi, Kenya.
11. Robin, H. (1993); **African since 1875 A modern History**, East African Publishers Ltd., Nairobi, Kenya.
12. Roland, O. and Anthony, A. (2007). **Africa since 1800**, Cambridge University Press, New York, USA.

13. History for Secondary Schools Form five (Tanzania Institute of Education)

14. History for Secondary Schools Form Six (Tanzania Institute of Education)

15. History for secondary schools: Form Five (TIE)

16. History for Secondary Schools: Form Six (TIE)

READING LIST FOR HISTORY TWO.

1. Nelson throne **Essential modern world history**

2. **History of 21st century** (World history) (Oxford)

3. H.L. Peacock. **A History of Modern Europe 1789-1981** seventh Edition (2010)

4. **The History of Modern World** (2007) 6th Edition by Oxford University Press.

GENERAL STUDIES

1. Richard, R.F. Mbalase. **General Studies For Advanced Level Certificate**;

2. Mgaywa, B.M. **General Studies for Advanced level 3rd Ed**.

3. Joannes BigirwaMungu & Sospeter.M. Deogratias. **Understanding Advanced Level general Studies;**

Advanced Secondary School Education;

GEOGRAPHY DEPARTMENT

1. (Colin Buckle), **LANDFORMS IN AFRICA**

2. C.R. KOTHARI), **RESEARCH METHODOLOGY**

3. (H.C. TRURAN), **A PRACTICAL GUIDE TO STATISTICAL MAPS AND DIAGRAMS**

4. (Goh cheng Leong.Gillian.C. Morgan), **HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY**

5. (DAVID WAUGH), **GEOGRAPHY-AN INTIGRATED APPROACH**.

6. (JOHN .M. PRITCHARD), **PRACTICAL GEOGRAPHY FOR AFRICA**

7. (R.B. BUNETTE), **PHYSICAL GEOGRAPHY IN DIAGRAMS FOR AFRICA**.

8. Geography for Secondary Schools form Five **(TIE)**

9. Geography for Secondary Schools Form six **(TIE)**

KWA WANAFUNZI AMBAO WATASOMA KEMIA NA NA ELIMU YA VIUMBE NA KEMIA

a. Chemistry

i). Advanced level organic chemistry by APE network 2012 ii).

A level secondary Education chemistry practical

iii). Advanced chemistry volume I and II by S. CHAND

iv). Environmental chemistry and pollution control by S.CHAND

v). Essential physical chemistry by S. CHAND

vi). Selected topics in inorganic chemistry by Wahid U. Malik et al vii). Organic chemistry by S.CHAND

B. **Biology**

i). CJ CLEGG with DG MACKEAN (2000) Advanced Biology principles and Application 2nd Ed,Hodder Murray London

ii). Sylvia S Mader (1996), Biology (5th Ed) Wm C. Brown publisher London

iii). DJ Taylor et al (1997), BIOLOGICAL SCIENCE, Cambridge university press — New York.

iv). MBV Roberts (1986), Biology A functional Approach (4th Ed)

v). Ann Fullick et al (2011), A level Biology, students Book, Longman.

N.B: Mzazi unashauriwa angalau kununua vitabu viwili kwa kila somo kwa ajili ya kumsaidia mtoto.

KARIBU SANA